Namba ya Mtahiniwa ____________________

**TUME YA KIKRISTO YA HUDUMA ZA JAMII**
**MITIHANI YA PAMOJA SHULE ZA MSINGI KANDA YA KASKAZINI**

**MTIHANI WA UTAMILIFU DARASA LA SABA 2024**

**02** **KISWAHILI**

**MUDA: Saa 1:40** **Alhamisi, Julai 11, 2024 Asubuhi**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali **Sita (6)**.
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
3. Majibu yote yaandikwe katika **karatasi hii.**
4. Tumia kalamu ya **bluu** au **nyeusi**.
5. Simu za mkononi na vifaa vingine visivyostahili **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika kwa usahihi **Namba yako ya mtihani** sehemu ya juu ya kulia kwenye kila ukurasa.

| KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **JINA LA MTAHINI** |
| **1.** | | |
| **2.** | | |
| **3.** | | |
| **4.** | | |
| **5.** | | |
| **6.** | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAINI YA MWINGIZA ALAMA** | | |



CamScanner

Namba ya Mtahiniwa______________________

## SEHEMU A ( Alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Sikiliza kwa makini hadithi utakayosomewa na msimamizi, kisha jibu kipengele cha **(i) – (v)** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku

   (i) Kutokana na habari uliyoisikiliza ni nani aliyezungumziwa ?
   (A) Amani (B) Bibi (C) Wananchi (D) Amani na bibi

   (ii) Amani alimuuliza swali gani bibi yake?
   (A) Kama unajua kuandika (B) Kama unajua kusoma na kuandika
   (C) Kama anajua kusoma (D) Kama anajua kuimba

   (iii) Amani anaishi katika kijiji cha Kikole . Je Amani anaishi na nani?
   (A) Bibi (B) Babu (C) Bibi na babu (D) Shangazi na njomba

   (iv) Kwa mujibu wa habari uliyoisikiliza . Amani anatabia gani?
   (A) Mvivu (B) Mdadisi (C) Mkarimu (D) Mchapakazi na mdadisi

   (v) Kichwa cha habari hii kinafaa kuwa kipi?
   (A) Kijiji cha Kikole (B) Amani (C) Amani na bibi yake (D) Bibi

2. **Katika kipengele cha (i) – (x), chagua jibu sahihi kutoka kwenye machaguo na kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye kisanduku**

   (i) Mmekula chakula? Mama aliuliza. Je, sentensi hii ipo katika nafsi ipi ?
   (A) Kwanza wingi (B) Pili wingi (C) Tatu umoja (D) Kwanza umoja

   (ii) **<u>La haula!</u>** Gari limeacha njia. Neno lililopigiwa mstari limetumika kama;
   (A) Kielezi (B) Kitenzi (C) Kihisishi (D) Kivumishi

   (iii) Mtoto aliyekuja jana ameondoka asubuhi, hii ni aina gani ya sentensi?
   (A) Ambatano (B) Sahihi (C) Shurutia (D) Changamoto

   (iv) Mashairi ya kimapokea yamegawanyika katika aina mbalimbali. Je ubeti wa shairi wenye mistari minne huitwaje ?
   (A) Mshororo (B) Tarbia (C) Kibwagizo (D) Mizani

   (v) **"Kuwa na nyota ya jaha"** maana yake ni:
   (A) Bahati nzuri (B) Bahati mbaya (C) Nyota ya asubuhi (D) Bahati nasibu

   (vi) "Wanakijiji wa Kilole hufanya kazi kwa kushirikiana" Ni methali ipi kati ya zifuatazo: inaweza kutumika kuwashauri wanakijiji hao kuendelea na ushirikiano ?
   (A) Dhahabu hupewa aliyeshinda (B) Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
   (C) Damu ni nzito kuliko maji (D) Lakuvunda halina ubani

   (vii) **"Watoto watukutu hufitiniana"** Kauli gani ya matendo inayojidhihirisha katika sentensi hiyo?
   (A) Kutendwa (B) Kutendeka (C) Kutendeana (D) Kutendea

   (viii) Mfuko umechanika. Katika sentensi hii neno **"Mfuko"** lipo katika ngeli ya
   (A) KI – VI (B) LI – YA (C) U – I (D) I - ZI



CamScanner

Namba ya Mtahiniwa ______________

(ix) Mali iliyofichwa ardhini hujulikana kama ______________
(A) Adhama (B) Fuadi (C) Nudhumu (D) Dafina

(x) Baba amelima shamba kubwa sana. Silabi inayoonesha nafsi ni ipi ?
(A) –li- (B) –a- (C) –me- (D) –lim-

3. **Panga sentensi zifuatazo kwa kuzipa mtiririko sahihi kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E**

(i) Kabla ya kuviondoa likaja jogoo likavisukuma. [ ]

(ii) Nilipomweleza mama hakunikaripia sana. [ ]

(iii) Mara tu baada ya kumaliza kula nikaviosha vyombo vyote na kuviweka juani ili vikauke. [ ]

(iv) Nikafurahi na nikarudi ndani kuendelea na kazi ya kujisomea. [ ]

(v) Vyombo vya udogo vyote vilivunjika. [ ]

4. Oanisha maneno yaliyopo katika **KIFUNGU A** na yale ya **KIFUNGU B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika mabano

| KIFUNGU A | MAJIBU | KIFUNGU B |
|---|---|---|
| (i) Pigwa na butwaa | [ ] | A. Danganya |
| (ii) Yamalishoni hayasimuliwi mjini | [ ] | B. Shangaa |
| (iii) Chotara | [ ] | C. Mtoto wa njiwa. |
| (iv) Visha kilemba cha ukoka | [ ] | D. Suriama |
| (v) Kipura | [ ] | E. Si vyema kuchanganya mambo |
| | | F. Msichana mrembo |
| | | G. Suria |

## SEHEMU B: (Alama 20)

5. **Soma Shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika sehemu zilizoachwa wazi**

Duniani kuna watu, wengi waliofanikiwa
Sio kwamba wana utu, kizidi niliopewa,
Ila si waoga katu, ndipo wamefanikiwa
Sitakubali kushindwa, lazima nifanikiwe.

Mambo yakiwa magumu, Kukata tamaa mwiko,
Shida zikizidi humu, waloshinda mbona wako,
Ninajipa majukumu, kupambana huko huko,
Sitakubali kushindwa, lazima nifanikiwe.

Sipungukiwi chochote, iweje nife masikini,
Akili ni mwili vyote, nimeshika mkononi,
Nawaza kwenda popote, kuishi humu nchini,
Sitakubali kushindwa, lazima nifanikiwe.



CamScanner

Namba ya Mtahiniwa________________

**Maswali**

(i) Mtunzi wa shairi hili anahimiza nini
(A) Elimu (B) Kupambana na maisha bila kukata tamaa
(C) Watu wengi ni waoga (D) Maisha mazuri tutayapata mbele ya safari

(ii) Mtunzi wa shairi hili unafikiri ni nani?
(A) Mtoto mdogo (B) Mwalimu (C) Mwanafunzi (D) Shaibu

(iii) Mshairi alikuwa na maana ipi aliposema "Akili na mwili vyote nimeshika mkononi
(A) Akili na nguvu anazo anatakiwa kuzitumia (B) Akili na nguvu anapaswa kuvihesabu
(C) Akili anazo aombe Mungu azitumie (D) Mwili na akili hufanya kazi moja

(iv) Katika ubeti wa pili vina vya kati na vya mwisho ni
(A) "Cho" na "ni" (B) "e" na "ni" (C) "mu" na "ko" (D) "le" na "ni"

(v) Kichwa cha shairi hili kwa maneno mawilí tu kinapaswa kuwa
(A) Sitakubali kushindwa (B) Lazima kusonga mbele
(C) Mwalimu na mwanafunzi (D) Ushindi lazima

## SEHEMU C: (Alama 10)

6. **Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata katika kisanduku ulichopewa**

Alikuwepo mtu mmoja aliyeitwa Kambanyuma. Alikuwa haoni kabisa na watu wengi waliamini ni kipofu. Siku moja Kambanyuma alikuwa anatembea barabarani kuelekea Kijiji cha Jirani . Mara akafika mahali ambapo barabara ina kona.Hapo kulikuwa na mwamba mkubwa ambao juu yake alitua kunguru. Kwa kuwa Kambanyuma alikuwa haoni vizuri akadhani kuwa ule mwamba ambao ni kunguru ni mtu aliyevaa kofia.

Je! bado mbali kufika Kijijini ? akauliza Kambanyuma na kutabasamu kungoja sauti. Je bado mbali kufika Kijijini? Kunguru kusikia vile akaogopa. Akapaa hadi kwenye tawi la mti akatulia kimya huku akijisawazisha juu ya lile tawi na kukaa chonjo endapo Kambanyuma ataamua kumdhuru. Kambanyuma kuona vile akacheka kidogo, kisha akasema kwa kuwa umekataa kunijibu na mimi sitakwambia kuwa kofia yako imepeperushwa na upepo.

**MASWALI**

(i) Kambanyuma alikuwa anatembea kuelekea wapi ?
(A) Kijiji cha jirani (B) Barabarani
(C) Kwenye mti alikotua kunguru (D) Kwenye kona ya barabara

(ii) Kambanyuma aliuliza tena "Je, bado mbali kufika kijijini?" Kunguru kusikia vile:
(A) Alijibu. (B) Alikimbia (C) Aliogopa (D) Alikaa kimya

(iii) Je, Kofia ilipeperushwa na upepo ?
(A) Kweli (B) Si kweli (C) Ikapotea (D) Ikatua juu ya mti

(iv) Mahali ambapo barabara ina kona kulikuwa na kitu gani ?
(A) Mto (B) Mwamba mkubwa ambao juu yake alitua kunguru
(C) Mti mrefu wenye matunda (D) Bonde la maji

(v) Watu wengi waliamini vipi kuhusu Kambanyuma ?
(A) Haoni vizuri (B) Ni kipofu (C) Chongo (D) Toinyo



CamScanner